*Makambako Mpya, Tuijenge pamoja*

TOLEO NA. 1

# MAKAMBAKO YETU

www.makambakotc.go.tz | Halmashauri ya Mji Makambako | Jarida la Robo ya pili oktoba- desemba 2022



*"Mkuu wa Wilaya ya Njombe,Mhe. Kissa Gwakisa Kasongwa akikagua madarasa ya Kidato cha kwanza 2023 Shule sita za Sekondari-Halmashauri ya Mji Makambako desemba 7,2022"*

**Jarida hili limeandaliwa:**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini- MakambakoTC **Tovuti:** www.makambakotc.go.tz



JARIDA oktoba - desemba 2022.indd 1 12/30/2022 6:55:26 AM



## DC AIPONGEZA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO KWA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MADARASA YA KIDATO CHA KWANZA 2023.

**M**kuu wa Wilaya ya Njombe, Mhe. Kissa Gwakisa Kasongwa ameipongeza Halmashauri ya Mji Makambako kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza 2023 kwa wakati na kwa kuzingatia ubora, na kumuagiza Mkurugenzi kumwandikia barua ya pongezi Mwenyekiti wa Mtaa wa Sigrid kwa kushiriki usimamizi wa ujenzi wa madarasa sita katika shule ya Makambako Sekondari iliyopo katika Mtaa anao uongoza.

Mhe. Kissa alitoa pongezi na agizo hilo  katika ziara ya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza 2023,katika shule sita za Sekondari za Halmashauri ya Mji Makambako desemba 7,mwaka huu.

Amesema kuwa katika miradi yote ya madarasa mwenyekiti wa Mtaa wa Sigrid,Bahati Nyato tangu mwanzo wa utekelezaji wa ujenzi wa madarasa amekuwa bega kwa bega na walimu katika usimamizi wa mradi bila kulazimishwa,kwani hata alipofanya ziara ya kushitukiza alimkuta eneo la mradi.

Aidha, Mhe. Kissa amesema ameridhishwa na kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo,kwani madarasa yamejengwa kwa ubora wa hali ya juu na uhakika wa wanafunzi kuyatumia madarasa hayo januari,2023 upo.

Ametoa agizo kwa Shule zote zenye ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza kukamilisha madarasa yote ndani ya muda uliopangwa,kabla ya tarehe ya mwisho ya kukabidhi madarasa ngazi ya taifa,kwa kuhakikisha umaliziaji wa baadhi ya vitu unakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa.

Halmashauri ya Mji Makambako ilipokea jumla ya Mil. 420 za ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023,ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa michango ya ujenzi wa madarasa.



JARIDA oktoba - desemba 2022.indd 2 12/30/2022 6:55:27 AM



## ZAIDI YA MIL. 264 ZA TASAF ZATUMIKA KATIKA UJENZI WA KITUO CHA AFYA KIJIJI CHA IKELU.

**W**ananchi wa Kijiji cha Ikelu. Kata ya Utengule katika Halmashauri ya Mji Makambako wameishukuru Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kutoa fedha zaidi ya Mil 264, zilizotumika katika ujenzi wa majengo matatu, jengo la wagonjwa wa nje,jengo la mama na mtoto na nyumba pacha za watumishi.

Mwenyekiti wa kijiji hicho Bw. Batson Nyagawa amesema kuwa,ujenzi wa Kituo hicho utawapunguzia wanachi mzigo wa gharama za matibabu kwani kwa sasa Kijiji cha Ikelu kina hospitali ya shirika la dini moja ambayo gharama za matibabu zipo juu tofauti na gharama katika hospitali na vituo vya Serikali.

Anna Mbangala,Mkazi wa Kijiji cha Ikelu na Mjumbe wa Serikali ya Kijiji amesema kuwa,ujenzi wa kituo cha afya katika Kijiji hicho una manufaa kwa jamii hasa kina mama kwani itawapunguzia gharama ya kupata huduma za uzazi,kwani kwa sasa mama mjamzito anatakiwa kulipia gharama za kujifunga kawaida kuanzia 50,000 na 250,000 upasuaji, hali inayowalazimu kufuata huduma hiyo Kituo cha afya Makambako kwani hakuna gharama zaidi ya kununua vifaa.

Mtendaji wa Kijiji cha Ikelu,Galous Myinga amesema kuwa hapo awali lengo lilikuwa kujenga Zahanati ya Kijiji kabla ya Serikali kuamuwa kujengwa kwa Kituo cha afya na walianza ujenzi wa majengo matatu ya rasmi mwezi april,2022 kupitia michango ya wananchi ambapo kwa wakati huo walifanikiwa kukusanya jumla ya Mil 16.7 na endapo wangejenga kupitia Michango ya wananchi pekee ujenzi hadi sasa ungekuwa hatua ya Msingi.

Ametoa shukurani kwa Serikali kwa kutoa fedha zilizofanikisha ujenzi wa majengo hayo,ambayo kwa sasa yapo hatua ya ukamilishaji pamoja na kuipandisha hadhi Zahanati hiyo Kuwa Kituo cha afya.

Mratibu wa TASAF katika Halmashauri ya Mji Makambako,Neema Chaula amebainisha Kutokana na mabadiliko ya Ujenzi wa Kituo cha afya badala ya Zahanati, Serikali Kupitia TASAF inatarajia kuongeza idadi ya majengo ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na jengo la upasuaji,Maabara na wodi ya mama na mtoto kwa gharama ya Mil. 135.



JARIDA oktoba - desemba 2022.indd 3 12/30/2022 6:55:28 AM



**Kamati ya fedha ya Halmashauri ya Mji Maambako Yaridhishwa na Usimamizi wa duka la dawa-Kituo cha afya Makambako.**

**K**amati ya Fedha na Uongozi ya Halmashauri ya Mji Makambako mnamo novemba 30,mwaka huu ilifanya ziara katika Kituo cha afya Makambako,na kutembelea duka la dawa lililopo katika kituo hicho na kufanya ukaguzi wa nyaraka za ununuzi na uuzaji wa dawa,matumizi sahihi ya mfumo pamoja na kusikiliza changamoto zinazojitokeza katika uendeshaji wa duka hilo.

Baada ya kupokea taarifa za duka hilo iliyowasilishwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Makambako, Dkt. Ally Senga Wahe. Madiwani wameridhishwa na mwenendo wa biashara ya dawa katika duka hilo,na kuupongea uongozi wa Kituo hicho kwa usimamizi bora.

Dkt. Senga amesema kuwa,uamuzi wa kuanzisha mradi wa duka la dawa kituoni hapo ulitokana na kukosekana kwa baadhi ya dawa kituoni hapo ambazo hutolewa kwenye hospitali,hali iliyowalazimu wagonjwa kununua dawa maduka ya nje kwa gharama kubwa,lakini pia kwa wagonjwa waliofika usiku wa manane walipata shida ya kutafuta dawa nje na kuhatarisha maisha yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya fedha na uongozi,Mhe. Hanana Mfikwa pamoja na wajumbe wa kamati hiyo wametoa ushauri kwa Uongozi wa kituo cha afya Makambako,Mfamasia na watumishi wanaohusika na uuzaji wa dawa katika duka hilo, kuweka kumbukumbu sahihi za takwimu za dawa zinazoingia na kutoka katika duka hilo , kwa kuandika katika daftari badala ya kutegemea mfumo pekee ili hata changamoto za kimfumo zitakapotokea takwimu ziwe salama.

Aidha,wametoa rai kwa Uongozi wa kituo hicho kuteua watumishi wachache ambao watakuwa na jukumu la kutoa huduma katika duka hilo pamoja na kulisimamia,ili kuepuka upotevu wa dawa na endapo hasara yoyote itajitokeza wawajibika kufidia.

Pia, Mhe. Hanana ametoa wito kwa Uongozi wa kituo hicho kuendelea kutoa elimu kwa wananchi, juu ya utendaji kazi wa duka hilo pamoja na umuhimu wake ili kuwajengea wananchi uelewa.

Dkt. Senga kwa niaba ya Uongozi wote wa kituo cha afya Makambako ametoa shukrani kwa pongezi za Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi na kuahidi kufanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa,ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa dawa kila mwezi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utendaji kazi wa duka hilo.

Duka la dawa la kituo cha afya Makambako linatoa huduma kama maduka mengine ya dawa yaliyopo mitaani,kwa kuuza dawa kwa bei nafuu kwa wagonjwa waliofika kupata huduma katika kituo hicho na wagonjwa wengine ambao wapo majumbani wenye uhitaji wa dawa wenye cheti cha daktari.




## Serikali yatoa vifaa vya Uchomeleaji kwa Vikundi Vya Vijana Nchini kukabiliana na soko la ajira.

**K**ikundi cha Vijana cha By Nature tech kutoka katika Mtaa wa Mlando,Kata ya Mjimwema katika Halmashauri ya Mji Makambako,kinachojishughulisha na kazi ya uchomeleaji vyuma kimekabidhiwa mashine tatu za kuchomelea na mashine tatu za kukatia vyuma,-zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana Ajira na Wenye ulemavu kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha vijana kujiajiri.

Akitoa taarifa ya mapokezi ya vifaa hivyo katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika novemba 25,2022 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii, Bi. Zuena Ungele amesema kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitoa maelekezo juu ya kutuma taarifa za vikundi vinavyofanya shughuli za uchomeleaji, kikundi cha By nature tech ni moja ya kati ya vikundi vilivyochaguliwa kuwa mnufaika wa mashine hizo.

Amesema kuwa, kikundi hicho chenye jumla ya vijana watano kilianzishwa mwaka 2021 na walipata mkopo wa mil 5 inayotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na kimefanikiwa kurejesha jumla ya shilingi mil 4.6 ndani ya muda na mnamo novemba 30,mwaka huu wanakamilisha deni lote.

Kabla ya kukabidhi mashine hizo,Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mhe. Hanana Mfikwa ameishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana,Ajira na Wenye ulemavu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kutoa mashine hizo ili kuwawezesha vijana kujiajiri na kuwapongeza vijana hao kwa kujitambua na kuweza kufanya marejesho ya mkopo vizuri na kuwataka kuendelea kutumia fedha wanazozipata kwa malengo,na kujiepusha na matumizi mabaya ya fedha wanazozipata kwa kufuata vipaumbele walivyojiwekea kufikia malengo yao.

Ametoa wito kwa Mkurugenzi kukitumia kikundi hicho katika kazi mbalimbali za uchomeleaji katika miradi inayotekelezwa na Halmashauri,ili kukiwezesha kikundi hicho kupata fedha.

Elichalido Ng'olo mmoja kati ya vijana watano wanaounda kikundi cha By nature tech, amemshukuru Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan,Makamu wa Rais,Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana,Ajira na Wenye ulemavu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuwapa mashine za uchomeleaji ambazo zitawasaidia kufanya kazi kwa uhakika kwani vifaa vya zamani vimechakaa.

Ametoa hamasa kwa vijana kuunda vikundi na kuaminiana ili waweze kupata mikopo kutoka Halmashauri, na kutumia fedha hizo kufanikisha malengo waliyojiwekea kwani fedha za mikopo ya Halmashauri zipo.




SHERIA NDOGO ZA LISHE KUANDALIWA ,KILA MTOTO APATE CHAKULA SHULENI.

**H**almashauri ya Mji Makambako inaandaa sheria ndogo kuhusiana na utoaji wa chakula shuleni na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya lishe ili kuhakikisha watoto wote wanapata lishe nyumbani na shuleni.

Tamko hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Kenneth Haule katika mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika oktoba 27,2022 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri,baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati ya uchumi,afya na elimu inayohusu hali ya utoaji wa chakula cha mchana katika shule za msingi,huku shule zilizopo Mjini zikiwa na idadi kubwa ya wanafunzi wasiopata chakula shuleni tofauti na shule zilizopo Vijijini.

Haule amesema kuwa kutokana na baadhi ya wazazi kukaidi kuchangia chakula cha watoto wao shuleni,Halmashauri inaandaa sheria ndogo kuhusiana na utoaji wa chakula shuleni na usimamizi wa utekelezaji wa mikataba ya lishe kuanzia ngazi ya Kijiji,Mtaa hadi Kata.

“Wazazi wanapaswa kutambua umuhimu wa chakula shuleni,suala sio mtoto apate chakula pekee,suala ni je,anapata chakula kwa muda sahihi? Na ni chakula gani? Jana tumesaini mikataba ya lishe pamoja na Watendaji wa Kata hivyo suala la chakula shuleni tunakoelekea sio hiyari tena itakuwa ni lazima kila mtoto kupata chakula shuleni chenye virutubisho muhimu kwa afya zao ikiwa ni agizo la Serikali”,alisema Haule.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako,Mhe. Hanana Mfikwa ameiagiza Kamati ya uchumi,afya na elimu pamoja na Idara ya elimu Msingi kuchakata uwiano wa miundombinu ya shule na idadi ya wanafunzi,ili kupata uwiano halisi na endapo hakuna uwiano hatua za kuongeza na kuboresha miundombinu zifanyike.




**B**araza la Madiwani limeridhia pendekezo la kuweka mkakati maalumu wa Halmashauri ya Mji Makambako la kutwaa maeneo makubwa pembezoni mwa Mji ili yatumike kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa shule na miradi mikubwa ya uwekezaji pamoja pamoja na uanzishwaji kwa Shule maalumu ya vipaji ya wanafunzi wa kike na shule ya sekondari ya kidato cha tano na sita ili kupunguza adha ya wanafunzi kukosa nafasi ya kuendelea na masomo baada ya kufaulu kidato cha nne.

Akiwasilisha pendekezo la Halmashauri kutwaa maeneo makubwa kwa ajili ya shughuli za kijamii na uwekezaji Mwenyekiti wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira, Mhe. Alimwimike Sahwi amesema kuwa kamati hiyo imetoa pendekezo hilo ili kupunguza changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya kulipa fidia badala yake,Halmashauri itwae maeneo ya watu na kuyapima na kugawana viwanja kwa utaratibu wa viwanja,asilimia 60 kwa mwenye eneo na asilimia 40 kwa Halmashauri kama gharama ya kufidia upimaji.

Mhe. Sahwi amesema kuwa,kwa utaratibu huo Halmashauri itaweza kuwa na miradi ya viwanja ambavyo inaweza kuuza na kupata fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kupata maeneo ya huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, masoko na vituo vya afya.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,afya na elimu,Mhe. Imani fute amewasilisha pendekezo la kamati hiyo la kuanzishwa kwa shule ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari Maguvani na shule ya vipaji maalumu ya wanafunzi wa kike wenye ufaulu mkubwa katika shule ya sekondari Mlowa kuanzia mwezi januari,2023 kwani shule hizo zina miundombinu inayowezesha uanzishwaji wa wa shule hizo.




**SERIKALI YATOA MASHINE ZA UCHOMELEAJI KWA KIKUNDI CHA VIJANA WA MTAA WA MLANDO.**

**K**ikundi cha Vijana cha By Nature tech kutoka katika Mtaa wa Mlando,Kata ya Mjimwema katika Halmashauri ya Mji Makambako,kinachojishughulisha na kazi ya uchomeleaji vyuma kimekabidhiwa mashine tatu za kuchomelea na mashine tatu za kukatia vyuma,zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana Ajira na Wenye ulemavu kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha vijana kujiajiri.

Akitoa taarifa ya mapokezi ya vifaa hivyo katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika novemba 25,2022 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii, Bi. Zuena Ungele amesema kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitoa maelekezo juu ya kutuma taarifa za vikundi vinavyofanya shughuli za uchomeleaji, kikundi cha By nature tech ni moja ya kati ya vikundi vilivyochaguliwa kuwa mnufaika wa mashine hizo zilizotolewa na Ofisi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana,Ajira na Wenye ulemavu kwa Halmashauri zote nchini.

Amesema kuwa, kikundi hicho chenye jumla ya vijana watano kilianzishwa mwaka 2021 na walipata mkopo wa mil 5 inayotolewa na Halmashauri kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na kimefanikiwa kurejesha jumla ya shilingi mil 4.6 ndani ya muda na mnamo novemba 30,mwaka huu wanakamilisha deni lote.

Kabla ya kukabidhi mashine hizo,Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mhe. Hanana Mfikwa ameishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana,Ajira na Wenye ulemavu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kutoa mashine hizo ili kuwawezesha vijana kujiajiri.

Amewapongeza vijana hao kwa kujitambua na kuweza kufanya marejesho ya mkopo vizuri na kuwataka kuendelea kutumia fedha wanazozipata kwa malengo,na kujiepusha na matumizi mabaya ya fedha wanazozipata kwa kufuata vipaumbele walivyojiwekea kufikia malengo yao.

Ametoa wito kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako kukitumia kikundi hicho katika kazi mbalimbali za uchomeleaji katika miradi inayotekelezwa na Halmashauri,ili kukiwezesha kikundi hicho kupata fedha na kuwataka vijana kuwa wabunifu na kufanya kazi zilizo ndani ya uwezo wao badala ya kazi za kufikirika.

Elichalido Ng'olo mmoja kati

ya vijana watano wanaounda kikundi cha By nature tech, amemshukuru Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan,-Makamu wa Rais,Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana,Ajira na Wenye ulemavu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuwapa mashine za uchomeleaji ambazo zitawasaidia kufanya kazi kwa uhakika kwani vifaa vya zamani vimechakaa.



Ametoa hamasa kwa vijana kuunda vikundi na kuaminiana ili waweze kupata mikopo kutoka Halmashauri, na kutumia fedha hizo kufanikisha malengo waliyojiwekea kwani fedha za mikopo ya Halmashauri zipo.





## HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO YASHIKA NAMBA 1 ZOEZI LA UTOAJI CHANJO YA POLIO MKOA WA NJOMBE.

**H**almashauri ya Mji Makambako imeshika nafasi ya kwanza awamu tatu mfululizo,katika kampeni za utoaji chanjo ya polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano  katika Mkoa wa Njombe.

Kauli hiyo ilitolewanovemba 29,2022 na mratibu wa Chanjo katika Halmashauri ya Mji Makambako, Bi. Tindichebwa Mazala katika kikao cha tathimini ya zoezi la kampeni za chanjo ya polio  zilizofanyika awamu tatu na utambulisho wa awamu ya nne ya kampeni ya chanjo ya polio itayoanza kutolewa desemba 1 hadi 4,2022 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Tindichebwa amesema kuwa matokeo ya kampeni zilizopita  yamefikia lengo ambapo awamu ya kwanza  watoto waliopata chanjo ni asilimia 144,awamu ya pili ni asilimia 125 na awamu ya tatu ni asilimia 120, na katika awamu ya nne ambayo ndiyo ya mwisho jumla ya watoto 33,496 wanatarajiwa kupata chanjo hiyo ili kukamilisha dozi.

Amesema kuwa,idadi hiyo ya watoto ambao ni walengwa wa kampeni ya chanjo awamu ya nne, inatokana na idadi ya watoto waliopata chanjo awamu ya tatu.

Ametoa wito kwa wazazi na walezi kuhamasika na kuhakikisha kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano,anapata chanjo ya polio  awamu ya nne ili kupata kinga kamili na kuachana na dhana potofu zilizojengeka katika fikra za baadhi ya watu.

Emmanuel George,Katibu Tawala Wilaya ya Njombe ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya afya ya msingi ametoa rai kwa wataalamu wa afya kuzingatia matumizi ya lugha rahisi,ili waweze kueleweka kwa wazazi na walezi wa watoto wanaotakiwa kupata chanjo hiyo kwa kutoa majibu sahihi juu ya utoaji wa chanjo ya polio kwa awamu nne.

Aidha, amewataka wataalamu wote wa afya wataoshiriki katika zoezi la utoaji chanjo nyumba kwa nyumba,kuwa wabunifu na kuzingatia muda na mazingira  ambayo wazazi na walezi  wanapatikana ili kihakikisha kila mtoto anapata chanjo hiyo ikibidi wafuatwe shuleni na maeneo mengine walipo kutokana na msimu wa kilimo.
Ametoa rai kwa wajumbe wote wa kikao cha kamati ya afya ya msingi kuhamasisha jamii na familia zenye watoto chini ya umri wa miaka mitano,ili watoto hao wapate chanjo ya polio awamu ya nne na kukamilisha dozi.

# MATUKIO KATIKA PICHA

**OKTOBA 2022- DESEMBA 2022**




TUZO YA UANDAAJI WA HESABU ZA MWISHO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.
Halmashauri ya Mji Makambako ilipata tuzo hii kwa kushika nafasi ya tatu katika kundi la Halmashauri 184 Nchini. Tuzo hizo zilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa hesabu Tanzania (NBAA)